**KARAMA YA UNABII**

“Mojawapo ya karama zinazotolewa na Roho Mtakatifu kwa kanisa lake ni karama ya unabii. Karama hii ni alama inayolitambulisha kanisa la Masalio na ilidhihirika katika huduma ya Ellen G. White. Kama mjumbe wa Bwana, maandishi yake yanaendelea kuwa chanzo madhubuti cha ukweli yanayotoa kwa kanisa faraja, uongozi, mafundisho, na maonyo. Pia yanaweka wazi kwamba Biblia ndiyo kanuni ambayo kwayo mafundisho yote na uzoefu lazima vipimwe.” (Yoe. 2:28, 29; Mdo. 2: 14-21, Ebr. 1: 13; Ufu. 12:17; Uf. 19:10)

**Karama ya Unabii nyakati za Biblia:**

Ijapokuwa dhambi ilikomesha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya Mungu na wanadamu (Isa. 59:1, 2; Kut. 20:18), Mungu hakukoma kuwasiliana na wanadamu. Alianzisha namna nyingine ya kuwasiliana na wanadamu kwa kupitia manabii (Ebr. 1:1-3, Uf. 1:1; Hes. 12:6). Katika Maandiko Matakatifu, nabii ni mtu ambaye hupokea mawasiliano kutoka kwa Mungu na kuwasilisha maudhui yake kwa watu wake Mungu. “Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2Pet. 1:21). Katika Agano la Kale, tafsiri ya nabii inatokana na neno la kiebrania nabi pale Mungu alipomwambia Musa kuwa amemweka kama Mungu kwa Farao na Haruni atakuwa nabii (Kut. 7: 1, 2). Majina mengine ni roeh (Isa. 30:10) au chozeh (2Sam. 24:11; 2 Falme 17:13). Zamani katika Israel mtu alipokwenda kuuliza jambo kwa Bwana alisema tukamwone mwonaji (1Sam.9:9). Neno ‘mwonaji’ hukazia kwamba mtu hupokea ujumbe kutoka kwa Mungu. Kwa miaka mingi, Mungu amekuwa akiwasiliana na mwanadamu kwa njia ya manabii (Amo. 3:7).

**Majukumu ya Manabii katika Agano Jipya:**

1. **Kusaidia Kuanzisha Kanisa:** Kanisa limejengwa kwa msingi wa mitume na manabii, Yesu Kristo akiwa jiwe kuu la pembeni (Efe.2:20, 21).

2. **Walianzisha Utume wa Kanisa:** Ni kwa njia ya manabii, Roho Mtakatifu aliwachagua Paulo na Barnaba kwa safari yao ya kwanza ya kiutume (Mdo. 13:1, 2) na akaelekeza ni wapi waende kufanya kazi (Mdo.16:6-10)

3. **Walijenga kanisa kiroho:** Lakini anayetoa unabii anasema na watu akiwajenga, kuwatia moyo na kuwafariji (1Kor.14:3). Pamoja na karama zingine za roho, unabii umetolewa kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma, ili kwamba mwili wa Kristo upate kujengwa.(Efe.4:12)

4. **Waliunganisha na kulilinda kanisa:** Manabii walisaidia umoja wa imani na kulilinda na mafundisho ya uwongo mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima kwa kufikia kipimo cha ukamilifu wa Kristo. Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa mafundisho kwa hila za watu, kwa ujanja, kwa kufuata njia zao za udanganyifu. (Efe.4:13,14)

5. **Walionya juu ya hatari zijazo:** Nabii moja katika Agano Jipya alionya juu ya njaa itakayokumba watu karibuni (Mdo.11:27-30) na wengine walionya kwamba Paulo atakamatwa na kufungwa Yerusalemu (Mdo. 20:23, 21:4, 10-14)

6. **Walithibitisha imani wakati wa ushindani:** Baada ya baraza la kanisa kuamua juu ya hoja za wokovu wa mataifa mengine, manabi walitumwa kwenda kuimarisha waumini. “Yuda na Sila, ambao wenyewe walikuwa manabii wakanena maneno mengi ya kuwatia moyo na kuwajenga katika imani wale ndugu walioamini.” (Mdo. 15:32)

**Karama ya Unabii katika Siku za Mwisho**

Wengine huamini kwamba karama ya unabii ilikoma wakati wa mitume kwenye Agano Jipya. Hata hivyo Biblia huthibitisha kuwepo kwa karama hii siku za mwisho. Hakuna ushahidi kwamba Mungu ataondosha karama ya unabii iliyotolewa ili kulijenga kanisa (Efe.4:13). Paulo anaonya watu wasimzimishe Roho na kuwataka waupime unabii (1Thes.5:19, 20). Anahimiza watu wapate kuhutubu (1Kor.14:1). Kukosekana kwa karama hii hakumaanishi kwamba Mungu amekoma kuzungumza na Kanisa bali kuwepo kwake kumeimarisha washiriki wakati wa taabu.

**Roho ya Unabii:**

Roho ya unabii ni karama ya unabii ambayo kupitia kwayo manabii wa zamani waliongea. “Katika habari ya wokovu huo manabii walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo.” (1 Petro 1:10-11). Roho ya Kristo ilishuhudia kupitia manabii. Ilikuwa ni ushuhuda wa Yesu kupitia kwa manabii ukielekezwa kwa kanisa la zamani.ni roho hiyo hiyo ya unabii ambayo Kristo aliitoa kama karama kwa kanisa la Agano Jipya. “Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu.” (Waefeso 4:11). Na kwenye Ufunuo 12 inawekwa wazi kuwa hii ni karama iliyohifadhiwa kwa ajili ya Kanisa la Waliosalia. Kanisa hili la siku za mwisho lilikusudiwa kuundwa na kuongozwa na Mungu kwa kazi maalumu ulimwenguni.

Mungu alipoliongoza kanisa lake kutoka Misri kwenda Kanaani aliweka karama ya unabii katikati yake. Ilikuwa ni kupitia karama hii ambapo msafara wote ulielekezwa na kuongozwa njiani. “Na kwa nabii Bwana alimtoa Israeli katika Misri, Na kwa mkono wa nabii alihifadhiwa.” (Hosea 12:13)

Msafara huo wa huko zamani umefananishwa na msafara (vuguvugu) mwingine wa injili utakaoishi siku za mwisho. Mungu atauinua tena mkono wake na kuwafufua masalio wa watu wake kutoka kona nne za dunia. “ “Na itakuwa katika siku hiyo, Bwana atapeleka mkono wake mara ya pili, ili ajipatie watu wake watakaosalia, kutoka Ashuru, na kutoka Misri, na kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu, na kutoka Shinari, na kutoka Hamathi, na kutoka visiwa vya bahari. Naye atawatwekea mataifa bendera, atawakutanisha watu wa Israeli waliotupwa, atawakusanya watu wa Yuda waliotawanyika, kutoka ncha nne za dunia.” (Isaya 11:11-12).

Kundi hilo la Waliosalia watakuwa wanatunza amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Kristo. Kundi hili la pili Mungu atalipatia karama ya unabii kama alivyofanya kwa kanisa lake la jangwani.  “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu . . .” (Ufunuo 12:17). Kwenye kitabu hicho hicho cha Ufunuo, neno ushuhuda wa Yesu lililotajwa hapa limefafanuliwa kama roho ya unabii. “Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii.” (Ufunuo 19:10)

Mungu analipatia kanisa la waliosalia jukumu la kuiinua amri kumi zilizokanyagwa na jukumu la kuhuisha karama ya unabii. Kwa mujibu wa Maandiko, Amri za Mungu na roho ya unabii vina uhusiano wa karibu sana. Pale maono ya kiunabii yanapokosekana watu huvunja sheria kama ilivyotokea kabla ya kuinuka kwa kanisa la Waliosalia. “Pasipo maono, watu huacha kujizuia; Bali ana heri mtu yule aishikaye sheria.” (Mithali 29:18)

**Roho ya unabii ilivyokuja**

Mwaka 1844 tunaelezwa kuwa mwanaume mmoja alitokewa na Mungu akimwonyesha safari ya Wanaomngoja Yesu wakielekea mji wa Mungu. Mtu huyu alipoambiwa asimulie maono hayo kwa wenzie alikataa akitoa udhuru kuwa kazi hiyo apewe mwingine. Mungu alimkubalia akamweleza kuwa mtu mwingine dhaifu zaidi amebebeshwa jukumu hilo. Siku moja akiwa anasikiliza nje ya mkutano akasikia mtu akisimulia maono kama yale yale aliyooneshwa, ndipo akawaambia watu kuwa maono hayo alipewa yeye kwanza lakini alikataa kusimulia. Aliyechaguliwa ni hakika alikuwa dhaifu wa wadhaifu kama Maandiko yasemavyo. “Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye nguvu.” (1 Wakorintho 1:27).

**Kuitwa kwa Ellen Harmon**

Mzigo wa karama ya unabii karibu na mwishoni mwa mwaka 1844 ulibebeshwa mabegani mwa binti mdogo aitwaye Ellen Harmon, aliyekuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakimngoja Yesu arudi Oktoba 22, mwaka huo wa 1844. Binti huyu akiwa anaomba kwenye maombi ya familia nyumbani kwake alitokewa na maono

Kama alivyotoa karama ya unabii kwa Yohana Mbatizaji amtambulishe Yesu kwa wanadamu, Mungu atatoa karama ya unabii ili kuja kwa Yesu mara ya pili kutangazwe kwa nguvu. Ni ukweli kwamba Yesu alitabiri ujio wa manabii wa uongo kabla ya ujio wake (Mt. 24:11, 24) na hili huashiria kwamba watakuwepo manabii wa kweli pia. Nabii Yoeli alitabiri kuwepo kwa ujazo wa Roho Mtakatifu ambao utatambulisha karama hii (Yoe: 2:28-31). Petro aliutumia unabii huu siku ya Pentekoste (Mdo. 2:2-21). Mvua ya masika hukomaza mazao (Yoel2:23) na kwa hiyo, ujio wa Roho Mtakatifu mwisho wa wakati utaimarisha imani (cf. Mt. 24:29; Uf. 6;12-17, Yoe. 2:31, Mt. 13:30, 39;) na yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokoka (Yoe.2:32)

**Karama ya Unabii katika Kanisa la Masalio**

Ufunuo 12 kinaonyesha vipindi viwili vya mateso kwa watu wa Mungu. Kipindi cha kwanza ni kile cha miaka 1260 ya mtu wa kuasi (Uf.12:6, 14). Kabla ya Yesu kurudi, masalio wenye kushika amri za Mungu na wenye ushuhuda wa Yesu watakasirikiwa na Shetani (Uf.12:17 Dan.12:1). Ule ushuhuda wa Yesu uko wazi katika mazungumzo ya Yesu na Yohana kwamba ni Roho ya Unabii (Uf.19:10 cf. Uf.22:9). Kukosekana kwa Roho ya Unabii kunafanya sheria ya Mungu idharauliwe (Omb. 2:9). Mungu alitoa karama ya unabii kuongoza watu wake waliotoka Misri (Mdo. 7:38, Hos.12:13). Watu wa Mungu kuihama dunia kutakamilisha unabii wa “Katika siku hiyo Bwana atapeleka mkono wake mara ya pili ili ajipatie watu wake watakaosalia” (Isa.11:11. 11)

**Kupima Karama ya Unabii**

Kwa kuwa watakuja manabii wa uwongo na wito wa Paulo kwamba “msitweze unabii, pimeni mambo yote, chagueni lililo jema (1Thes.5: 20-22 cf. 1Yoh. 4:1), ni vema kuwa na vigezo vya kuwapima manabii, tujue kwamba wametumwa na Mungu. Vigezo vifuatavyo vinafaa sana:

1. **Je ujumbe unakubaliana na Biblia?** “Na waende kwa sheria na ushuhuda, kama hawasemi sawasawa na neno hili ni kwa sababu hao hakuna asubuhi” (Isa.8:20 cf. Kumb.13:1-4) Roho za manabii hutii manabii (1Kor. 14:32) na pia kwa Mungu hakuna kugeuka geuka (Yak.1:17).

2. **Je atabiricho kinatimia?** Tutajuache kwamba huyu ametumwa na Bwana, ni kwamba anachosema ni lazima kitimie (Kumb.18:21, 22 cf. Jer. 28: 9). Hata hivyo ni vema kuzingatia unabii wenye masharti (Jer. 18:7-9).

3. **Je, anatambua kufanyika mwili kwa Kristo?** Akikiri Yesu amekuja katika mwili atakubalika, akikataa basi hakubaliki (1Yoh. 4:1-3).

4. **Je, nabii ana matunda mema au mabaya?** Kwa kuwa unabii unatoka kwa Mungu (2Pet. 1:21) lazima matunda yake yawe mema. "Mtawatambua kwa matunda yao" (Mt. 7:16, 18-20). Eliya alikuwa na hali ya kibiunadamu (Yak.5:17) hata hivyo, maisha yake hayakuwa ya kimwili bali yalijawa na tunda la roho (Gal. 5:19-22). Pili, matokeo yake kazi ya nabii daima ni kulisaidia kanisa (Efe.4:12-16)

**Roho ya Unabii katika Kanisa la Waadventista Wasabato**

Karama ya unabii ilijidhihirisha katika huduma ya Mama Ellen G. White, mojawapo ya waanzilishi wa Kanisa. Tangu mwaka 1844 alipokuwa na miaka 17 hadi mwaka aliofikwa na mauti 1915, alipata maono zaidi ya 2,000. Alifanya kazi Marekani, Ulaya na Australia akishauri, akifungua kazi, akihubiri na kuandika. Kwa kumpima kwa vigezo tulivyobainisha, anatosheleza kabisa.

1. **Kukubaliana na Biblia:** Kazi yake ya uandishi imenukuu aya maelfu za Biblia, mara nyingi yakifafanuliwa. Uchunguzi makini umedhihirisha kwamba maandiko yake yanalingana, ni sahihi na yanapatana kabisa na Biblia.

2. **Usahihi wa Utabiri:** Ellen alitabiri mengi na mengine yanasubiri kutimizwa. Hata hivyo, yaliyotimia ni (1) Kuinuka kwa umizimu – mwaka 1850 wakati umizimu unaanza alionya kwamba ni udanganyifu utakaoendelea hadi siku za mwisho. (2) Ushirikiano wa karibu baina ya Ukatoliki na Uprotestanti (3) Kazi ya kuchapa vitabu, kwamba mwanzo wake ni mdogo lakini hatimaye utafaulu.

3. **Kumkiri Yesu katika mwili:** Katika kitabu chake cha Tumaini la Vizazi Vyote (Desire of Ages) Mama White amekiri kwamba Yesu amekuja katika mwili. Pia kwenye kitabu cha Njia Salama (Steps to Christ) anamkiri Yesu.

4. **Mvuto wa Kazi yake:** Zaidi ya karne na nusu imepita tangu afariki, lakini maoni haya yanawakilisha vema mguso wake:

"Ingawa hakuwa ofisa wa kanisa wala hakupokea mshahara hadi mume wake alipofariki, kando ya Biblia, huduma yake ndiyo imeunda sura ya Kanisa la Waadventista wa Sabato." Richard Hammill, Karama za Roho katika Kanisa Leo, Ministry Julai 1982.

**Roho ya Unabii na Biblia**

Maandiko ya Ellen White siyo badala ya Maandiko Matakatifu. Haiwezekani kuwekwa kwenye ngazi sawa. Maandiko Matakatifu husimama peke yake, kiwango pekee cha kupima mafundisho yote pamoja na maandishi ya Ellen White.

1. **Biblia kipimo pekee:** Waadventista Wasabato huamini katika kanuni ya Sola Scriptura kwamba Biblia na Biblia peke yake ndiyo mtafsiri wake, na msingi wa mafundisho yote. Kanisa halikupokea mafundisho yake kutoka kwa Ellen White ila kutoka kwenye Biblia. Huduma yake ilisaidia kuelewa Biblia na kuthibitisha hitimisho lililofikiwa kwa kusoma Biblia.

2. **Kuongoza Kwenye Biblia:** Yeye mwenyewe aliona kazi yake kuwa ni kuongoza watu kurudi kwenye Biblia, kwa kuwa watu walikuwa wameacha kuifuata.

3. **Kuongoza kuelewa Biblia:** Ellen White aliona kuwa mafundisho yake yanasaidia mtu kuelewa vema Biblia. Shuhuda zilizotolewa siyo nuru mpya, bali hukazia nuru iliyokwisha kutolewa yaani Biblia.

4. **Kuongoza kutumia Kanuni za Biblia:** Unabii wa Ufunuo utadhihirika pale ambako kila moja atapima na kuchukua kilicho chema. Twaweza kupata au kupoteza kulingana na jinsi tunavyochunguza Maandiko.

**Historia ya Ellen White:**

1. Alizaliwa Novemba 26, 1827 shambani Gorham, Maine, kama maili 12 kutoka Portland. Akiwa na pacha mwenzake, alikuwa mdogo kuliko wote katika familia yenye watoto wanane. Alikuwa mtoto mwenye furaha akipenda sana mambo ya imani.

2. Maisha yake yalibadilika siku moja wakati akiwa anavuka Park alipopigwa jiwe na msichana mwingine. Pua yake ilivunjika na uso wake uliharibika kwa muda. Alizimia wiki tatu na mshtuko ulimfanya asiweze kufanya chochote kwa wakati mrefu. Kusoma kwake kulikoma kwa kuwa afya yake haikuruhusu.

3. Mwaka 1840 hadi mwaka 1844 Ellen na familia yao walisikiliza mahubiri ya William Miller, juu ya ujio wa Yesu ulivyo karibu. Walikubaliana na mahubiri na hawakuhama kutoka kwenye kanisa lao la Methodist. Hata hivyo haikuwa rahisi. Katika mkutano wa kambi mojawapo, alijitoa na ndipo roho yake ilipotulia. Tangu wakati huo alianza mahusiano mapya na Bwana wake.

4. Familia yake ilikubali Kilio cha Usiku wa Manane na kuacha makanisa yaliyoasi – yaani yaliyokataa ujumbe wa Yesu kurejea mara ya pili. Pamoja na kwamba Yesu hakurudi kama walivyotarajia, hawakukata tamaa kuacha imani yao.

5. Maono yake ya kwanza yalikuja muda mfupi baada ya mategemeo yao ya Yesu kurejea kutokutimizwa. Akiwa na umri mdogo (miaka 17), uwezo wake mdogo kuongea, afya yake iliyozorota, na kipindi kigumu alichokabiliana nacho, alimwomba Mungu amwepushe na jukumu la kuwa mjumbe wake. Hata hivyo wito wake haukubadilishwa, na hivyo alikubali kufanya kile ambacho Mungu alimwamuru.

6. Apili Mwaka 1847 alipewa njozi ya Sabato. Aliona Hekalu mbinguni Yesu akifungua pazia. Kwenye Patakatifu pa Patakatifu, aliona Amri Kumi za Mungu na mng'ao wa mwanga ukimulika amri ya nne, ambayo ni Sabato. Akajulishwa kwamba kama Sabato ingeendelea kutunzwa kwa uaminifu na wanadamu, asingekuwako asiyeamini Mungu, wenye mashaka na ulimwengu usingeingia kwenye ibada ya sanamu. Njozi hii, ilifungua mlango wa kuhubiri ujumbe wa Malaika wa Tatu kwa nguvu. Waumini walioona umuhimu wa Patakatifu, Sabato na Ujio wa Yesu mara ya pili, walikuja kuwa waanzilishi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato. (Life Sketches pp. 95)

7. Kwa miaka 70 iliyofuata, jukumu lake lilikuwa kupokea mashauri kutoka kwa Mungu naye aliyatoa kwa watu wake. Alizungumza katika mikutano mingi na aliandika vitabu vipatavyo 40 ambavyo vilikuja kujulikana kama Roho ya Unabii, akachangia pia kuchapisha makala nyingi katika machapisho ya kanisa la Waadventista wa Sabato. Kitabu kinachopendwa zaidi ni habari za maisha ya Yesu – Tumaini la Vizazi Vyote. Alisafiri kuzunguka sehemu nyingi za Amerika Kaskazini, Ulaya, Australia na New Zealand, akifungua kazi katika maeneo mapya. Alikuwa muhimu katika kufungua chuo cha Avondale kilichoko Australia.

8. Ellen White alipokea ujumbe kwa njia ya maono. Katika maono, uko ushahidi kwamba aliongozwa na Mungu. Aliangalia vitu vilivyo mbali, kuhema kwake kulikoma lakini hakubadilika rangi wala moyo wake haukukoma kudunda. Shuhuda za waliomwona, pamoja na madaktari, walishuhudia kwamba utaratibu wote haukuwa wa kidunia. Kuna wakati alibeba Biblia kubwa ya paundi 18 kwa nusu saa pasipo kuyumba wala kuidondosha.

9. Baadhi ya vitabu alivyoandika ni Shuhuda kwa Kanisa (1855-4909), Early Writings (1882), The Great Controversy (1888), Patriarchs and Prophets (1890), Gospel Workers (1892), Steps to Christ (1892), Thoughts from the Mount of Blessings (1896), Christ's Object Lessons (1900), Education (1903), The Ministry of Healing (1905), The

Acts of Apostles (1911), Counsels to Parents, Teachers and Students (1913), Prophets and Kings (1916).

10. Ellen White alilala usingizi wa mauti nyumbani kwake Elmshaven Julai 16, 1915 akazikwa alikozikwa mume wake na watoto wake Battle Creek.